



ISO 9001: 2008 CERTIFIED

IDARA YA FORODHA NA USHURU WA BIDHAA

TAARIFA KWA UMMA

UTOAJI WA TAARIFA KUHUSU FEDHA TASLIMU NA HATI ZA MALIPO ZINAZOSAFIRISHWA KUINGIA NCHINI AU KUTOKA NJE YA NCHI

Taarifa inatolewa kwa umma kwamba Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu, Sura 423 na Kanuni yake inayohusu utoaji wa taarifa ya kiasi cha fedha taslimu na Hati za Malipo zinazosafirishwa kuingia au kutoka nchini zimeipa Mamlaka ya Mapato Tanzania mamlaka ya kusimamia utoaji wa taarifa kuhusu fedha zinazosafirishwa kuingia au kutoka nchini. Taarifa hii inahusu usafirishaji wa fedha taslimu au hati za malipo (Bearer Negotiable Instruments) zinazofikia au kuzidi dola za kimarekani 10,000 (elfu kumi) au fedha nyingine yoyote yenye thamani sawa na hiyo iwapo fedha au hati hizo zitasafirishwa kwa njia zifuatazo

- (a) mtu yeyote anayesafiri akiwa nazo au katika mizigo anayoambatana nayo au katika chombo cha usafiri;
- (b) katika makontena ya kubebea mizigo, na
- (c) kwa njia ya vifurushi.

Kutokana na mamlaka iliyopewa kisheria, Mamlaka ya Mapato Tanzania inachukua fursa hii kuutaarifu umma kuwa, kuanzia tarehe 01 Oktoba 2017, msafirishaji yeyote wa fedha taslimu au hati za malipo zinazofikia kiwango kilichotajwa na kanuni hizi atalazimika kutoa taarifa kwa kujaza fomu zitakazopatikana kwa maafisa forodha mipakani. Ni vyema umma ukafahamu kuwa kutotoa taarifa au kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu usafirishaji huo ni kosa kisheria

Kwa taarifa au ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa namba za simu za bure: 0800 750075 au 0800 780078, au Barua pepe: huduma@tra.go.tz

Ifahamike kuwa, utaratibu huu haukusudii kuzuia usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo kuingia au kutoka nchini.

‘Pamoja Tunajenga Taifa Letu’

George I. Mnyitafu

KAIMU KAMISHNA WA FORODHA NA USHURU WA BIDHAA